RIPOTI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA USTAWI WA JAMII YA

BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha106(e) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012. Majukumu ya Kamati yameelezewa katika kanuni ya 112 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi ambapo miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kama yafuatayo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizoya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka ulitangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswaada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika .

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ina jukumu la kufuatilia utekelezaji katika Wizara tatu nazo ni kama ifuatavyo:-

1) Wizara ya Afya

2) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

3) Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 ilifanya kazi zake Unguja kwa muda wa wiki sita.

I. Wiki mbili za mzunguko mwanzo kuanzia tarehe 09/09/2013 - 20/09/2013.

II. Wiki mbili za mzunguko wa pili kuanzia tarehe 18/11/2013 – 29/11/2013.

III. Wiki mbili za mzunguko wa mwisho kuanzia tarehe 30/12/2013 – 10/01/2014.

Hata hivyo, kabla ya kuanza kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ilifanya kazi kwa muda wa wiki mbili Pemba kuanzia tarehe 13/05/2013 hadi tarehe 24/05/2013. Lengo la kazi hiyo ni kufuatilia utekelezaji wa Bajeti katika Idara na Taasisi za Serikali katika kipindi cha Aprili- Juni 2012/2013.

WAJUMBE WA KAMATI

Kamati ina wajumbe saba na makatibu wawili kama wafuatavyo-:

1.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hassan Hamad Omar	Makamo Mwenyeki
3.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe.
4.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	Mjumbe.
5.	Mhe. Farida Amour Mohamed	Mjumbe.
6.	Mhe. Mohamed Mbwana Hamad	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaid Kassim Mussa	Mjumbe
8.	Ndg. Maryam Rashid Ali	Katibu
9.	Ndg. Asha Said Mohamed.	Katibu

SEHEMU YA PILI

WIZARA YA AFYA

Wizara ya Afya imeundwa na Idara zifuatazo:-

1. Idara ya Kinga na Elimu ya Afya.
2. Idara ya Tiba.
3. Idara ya Hospitali ya Mnazi mmoja.
4. Idara ya Bohari kuu ya Dawa.
5. Idara ya Sera, Mipango na Utafiti.
6. Idara ya Utumishi na Uendeshaji.

Pia Wizara ina Taasisi Maalum ambazo miongoni mwao ni Chuo cha Taaluma za sayansi za Afya, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Baraza la wauguzi na Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala.

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA.

Idara hii ina jukumu la kuhakikisha utolewaji wa huduma bora za kinga pamoja na elimu ya afya kwa wananchi ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Kamati ilipofanya kazi ilipatiwa maelezo juu ya utekelezaji wa majukumu mbali mbali ya Idara.

KITENGO CHA MARADHI YASIYOAMBUKIZA.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITENGO CHA MARADHI YASIYOAMBUKIZA.

1. Kitengo kinakabiliwa na uchache wa wafanyakazi ambapo wafanyakazi waliopo ni wawili na mahitaji ni wanne. Hali hiyo inapelekea wafanyakazi kuwa na majukumu mengi na kuchukua muda wao wa ziada katika kuyakamilisha majukumu hayo.

2. Jamii kukosa taaluma ya kutosha juu ya namna ya kugundua dalili za magonjwa yasiyo ya kuambukiza na pia wahudumu wa afya kutokuwa na taaluma ya kutosha katika kutibu magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

3. Jamii kubadilisha mfumo wa maisha na kuishi katika mtindo unaochangia watu kupata magonjwa yasiyoambukiza kama vile kutokula mlo kamili, ongezeko la matumizi ya

tumbaku, kuacha kufanya mazoezi na mambo mengineyo ambayo hupelekea ongezeko kubwa la maradhi yasiyo ya kuambukiza.

4. Ongezeko la matumizi ya dawa za kienyezi zinazoelezwa kuwa zinatibu magonjwa kama ya kisukari, saratani, shindikizo la damu na kadhalika ambazo ukweli na ubora wake hazijathibitishwa na vyombo husika.

5. Tatizo la Upatikanaji wa taarifa za magonjwa kutoka katika vituo vya afya na kliniki za magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

6. Upatikanaji wa huduma za magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa baadhi ya vituo vya afya vya daraja la kwanza na la pili sio mzuri.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya ili waweze kugundua na kutibu magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa mujibu wa miongozo mbali mbali ya afya na pia inaishauri Wizara kuendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia njia tofauti zitakazoweza kufikisha ujumbe kwa ufanisi juu ya njia za kujikinga na magonjwa hayo.

2. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuisaidia Wizara katika kuhakikisha kuwa huduma za magonjwa yasiyo ya kuambukiza zinaimarika katika ngazi zote.

KITENGO CHA KUPAMBANA NA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITENGO CHA KUPAMBANA NA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE.

1. Kitengo kukosa mchango wa fedha kutoka Serikalini; fedha zote zinazotumika kutekeleza shughuli zao mbali mbali zinatokana na mchango wa wafadhili pekee.

2. Kitengo kinakabiliwa na matatizo ya kuvunjiwa na kuibiwa kwa baadhi ya vifaa kutokana na kukosekana kwa uzio katika jengo lao.

3. Jamii kutokuwa na muamko katika kutumia dawa za kichocho ambazo gharama yake ni kubwa hali inayopelekea upotevu wa fedha za Serikali katika kununua dawa hizo na huku jamii ikishindwa kuzitumia ipasavyo.

4. Pia Kitengo kukosa wataalamu ambapo watendaji wengi waliopo elimu zao ni za kiwango cha chini na hukosa fursa za kujiendeleza.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

Kamati inaitaka Wizara kuizungushia uzio ofisi ya Kitengo cha magonjwa yasiyopewa kipaumbele iliyopo Mianzini ili kudhibiti wizi wa rasilimali za ofisi na pia Kamati inaitaka Wizara kuchukua jitihada za kuelimisha jamii umuhimu wa kutumia dawa za kichocho ambazo gharama yake ni kubwa lakini jamii imekosa muamko wa kuzitumia dawa hizo.

KITENGO CHA AFYA YA WAFANYAKAZI.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITENGO CHA AFYA YA WAFANYAKAZI.

1. Ufinyu wa Ofisi: kuna chumba kimoja tu ambacho hutumika kwa shughuli zote za kuwahudumia wafanyakazi na wakati mahitaji ilikuwa vipatikane vyumba vinne ambavyo vitumike kwa shughuli mbali mbali za uchunguzi wa afya za wafanyakazi.

2. Kukosekana kwa usafiri wa Kitengo hali inayopelekea wafanyakazi wa Kitengo kushindwa kufanya kazi za nje na hatimae kubakia hapo hapo katika kitengo kwa ajili ya kuwahudumia wafanyakazi watakaofuata huduma hizo.

3. Uchache wa wafanyakazi ambapo wafanyakazi waliopo ni wanane na mahitaji ni kumi na tano.

4. Uchakavu wa vitendea kazi na vifaa mbali mbali vya Kitengo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

Kamati inaitaka Wizara kuipatia usafiri wa uhakika Kitengo cha Afya ya wafanyakazi ili kiweze kutekeleza shughuli zake mbali mbali ikiwemo za ukaguzi wa sehemu za kazi, kufanya uchunguzi wa afya za wafanyakazi na kutoa elimu ya afya katika taasisi tofauti zikiwemo za Serikali na za Binafsi.

KITENGO CHA LISHE.

Kamati ilipotembelea Kitengo iliarifiwa kuwa Kitengo kinaendelea na majukumu ya kupanga, kutekeleza, kusimamia, kutathmini na kufuatilia shughuli za lishe nchini. Katika kufanikisha majukumu yao Kitengo kinaendelea na shughuli za kuielimisha jamii juu ya ulaji bora, kupambana na ukosefu wa vitamini na madini pamoja na utekelezaji wa matibabu ya utapiamlo mkali hususani kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITENGO CHA LISHE.

1. Kamati ilibaini kuwa Kitengo kina uchache wa fedha katika utekelezaji wa majukumu yake hali inayopelekea Kitengo kutegemea sana fedha za wafadhili. Aidha, iwapo fedha za wafadhili zitapokosekana kazi hushindwa kufanyika kutokana na kuwa fedha zinazoingia kutoka Wizarani ni chache na huchelewa kuingia hali inayokwamisha utekelezaji wa kazi kwa mujibu walivyojipangia.

2. Kamati ilibaini kuwa ukusanyaji wa takwimu za watoto walio chini ya umri wa miaka mitano zinazohusiana na utapiamlo mkali imekuwa ni tatizo; kwa vile vituo vya afya vimekuwa haviweki takwimu vizuri na kupelekea kukosekana kwa takwimu sahihi.

3. Kamati iligundua kuwa utekelezaji wa matibabu ya utapiamlo bado ni tatizo kwasababu baadhi ya wanajamii wamekuwa na imani potofu za kuwapeleka watoto wao kwa waganga pindi wanapougua badala ya kuwapeleka katika vituo vya afya.

4. Kamati iliarifiwa kuwa kuna upungufu wa wafanyakazi wa fani ya lishe kwenye Wilaya ambapo maafisa afya ya jamii ndio wanaotumika katika kuhudumia Wilaya zilizo na upungufu huo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa Kitengo kinapatiwa fedha za kutosha ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwani kutegemea wafadhili pekee kunazorotesha utekelezaji wa majukumu ya Kitengo.

2. Kamati inaiagiza Wizara kuvisimamia Vituo vya Afya kwa kuhakikisha kuwa takwimu za watoto walio chini ya umri wa miaka mitano zinazohusiana na utapiamlo mkali zinawekwa vizuri ili utekelezaji wa matibabu ya utapiamlo mkali uwe kwa ufanisi na pia kuishajihisha jamii kuwapeleka watoto katika vituo vya afya kwa ajili ya kupata matibabu mapema pindi watakapogundua kusumbuliwa na maradhi mbali mbali ikiwemo utapiamlo.

3. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa wanaajiri wafanyakazi wenye Fani ya Lishe katika Wilaya zilizo na upungufu ili hatimae waweze kuhudumia Wilaya ipasavyo.

KITENGO CHA HUDUMA ZA MATIBABU YA MACHO.

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Kitengo cha Macho ambacho miongoni mwa majukumu yake ni kuikinga jamii kutokana na maradhi mbali mbali ya macho pamoja na kutoa tiba sahihi inayohusiana na maradhi ya macho.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KITENGO CHA HUDUMA ZA MATIBABU YA MACHO.

1. Kukosekana kwa jengo: Kamati ilibaini ufinyu wa nafasi katika jengo la Hospitali ya Macho hali inayopelekea wafanyakazi na wagonjwa kujibana katika maeneo finyu yaliyopo.

2. Kamati ilibaini uhifadhi mbaya wa vifaa vya matibabu ya macho ambao unatokana na ufinyu wa nafasi na kupelekea kuharibika kwa vifaa kama kifaa cha visual field analyser na laser mashine.

3. Kukosekana kwa gari la wagonjwa na dereva. Kamati ilibaini gari linalotumika kusafirishia wagonjwa kutoka hospitali ya Macho iliyopo kwa Mtipura mpaka Hospitali ya Mnazi mmoja ni gari la Mradi na kutokana na kukosekana kwa dereva wa gari hiyo, Daktari anaetibu wagonjwa wa macho analazimika pia kuwa dereva wa gari hilo.

4. Kukosekana kwa fedha za bajeti kwa Kitengo hupelekea kutegemea fedha za wafadhili pekee kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Kitengo hicho.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuipatia jengo la kutosha Hospitali ya Macho ili iweze kutoa huduma za matibabu ya macho kwa ufanisi na kuweza kuhifadhi vyema vifaa vya Hospitali.

2. Kamati inaitaka Wizara kupitia bajeti yake wakipangie Kitengo cha macho mgao wa fedha za bajeti ili waondokane na utegemezi wa wafadhili moja kwa moja na pia kulitafutia ufumbuzi swali la usafiri na dereva katika Hospitali ya Macho.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA.

HOSPITALI YA MNAZI MMOJA.

CHANGAMOTO INAYOIKABILI HOSPITALI YA MNAZI MMOJA.

1. Hospitali ya Mnazi mmoja inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendea kazi na vifaa vikiwemo vitanda vya kubebea wagonjwa na viti hali ambayo hupelekea usumbufu kwa wagonjwa na wafanyakazi hospitalini hapo.

2. Kukosekana kwa kifaa cha DNA PCR mbacho hutumika kwa kupimia damu za watoto ambao wamezaliwa na mama walioambukizwa VVU hali inayopelekea damu za watoto hao kusafirishwa kwenda hospitali ya Muhimbili kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na

ambapo kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa majibu.

3. Kukosekana kwa tanuri la kuchomea taka taka za hospitali (incinerator) ambapo taka taka huchomwa ufukweni mwa bahari ubavuni mwa Hospitali na kusababisha uharibifu wa mazingira pamoja na kuhatarisha maisha ya viumbe.

KITENGO CHA TAKWIMU ZA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

4. Ufinyu wa nafasi na miundombinu ya umeme kutokidhi haja: hali inayopelekea utunzaji wa mafaili ya wagonjwa kuwa katika utaratibu mbaya usiofahamika, upotevu wa kumbukumbu za wagojwa na usumbufu mkubwa pindi mgonjwa anapohitaji kumbukumbu zake. Aidha, kutokana na miundombinu ya umeme kuwa mibaya katika chumba hicho inakuwa vigumu sana kuweza kuzipata taarifa za mgonjwa pindi kiza kinapoingia.

5. Uchache wa mafunzo kwa watendaji wa Kitengo hupelekea watendaji kukosa kuenda sambamba na taaluma ya uhifadhi wa kumbukumbu kulingana na mabadiliko yaliyopo ulimwenguni.

6. Upungufu wa wafanyakazi ambapo wafanyakazi waliopo ni sita na mahitaji ni kumi na mbili. Kitengo kinatakiwa kifanye kazi muda wote wa masaa ishirini na nne ili inapotokea haja ya mgonjwa kuhitaji kumbukumbu zake apatiwe kwa wakati lakini kutokana na upungufu uliopo watendaji humudu kuwepo kazini mpaka muda wa saa tatu usiku.

HOSPITALI YA WAGONJWA WA AKILI

CHANGAMOTO INAYOIKABILI HOSPITALI YA WAGONJWA WA AKILI

1. Upungufu wa wafanyakazi katika ngazi ya madaktari, wauguzi, walinzi, wasafishaji na wapishi hivyo kupelekea waliopo kuzidiwa na majukumu.

2. Ufinyu wa bajeti ya chakula ambapo fedha zinazopatikana kwa mwezi ni shilingi milioni mbili tu au chini ya hapo na wakati mahitaji halisi ni shilingi milioni sita. Hivyo Bajeti hiyo ndogo hupelekea wagonjwa kupatiwa mlo mmoja tu kwa siku ambao huwa si mlo kamili kwa mahitaji ya wagonjwa hao.

3. Gari ya kuhudumia hospitali kukosa mafuta na hivyo gari hilo hubakia hospitalini hapo bila ya kutoa huduma yeyote.

4. Upungufu wa dawa muhimu hupelekea wagonjwa kukosa kuendeleza dozi zao kama inavyotakiwa.

5. Uchakavu wa jengo ikiwemo hali mbaya ya vyoo, makaro na wodi za wagonjwa.

HOSPITALI YA MWEMBELADU.

CHANGAMOTO INAYOIKABILI HOSPITALI YA MWEMBELADU.

1. Ufinyu wa nafasi katika sehemu ya kuwahudumia waathirika wa virusi vya ukimwi hali inayopelekea waathirika hao kusubiria huduma katika sehemu ya nje iliyowazi.

2. Uchakavu wa baadhi ya vifaa vya hospitali kama mashine ya Ultra sound na mashine ya kufulia katika sehemu ya kufulia.

3. Kukosekana kwa madaktari katika hospitali hali inayopelekea wauguzi kutoa huduma zote kwa wagonjwa.

4. Kukosekana kwa chakula cha wagonjwa kwa muda mrefu ambapo Kamati ilarifiwa kuwa imeshafika miezi nane bila ya kupatikana chakula cha wagonjwa hospitalini hapo.

5. Kukosekana kwa uzio na walinzi katika hospitali hali inayohatarisha usalama wa wafanyakazi waliopo hospitalini na ukizingatia kuwa asilimia kubwa ya wafanyakazi ni wanawake.

6. Kukosekana kwa gari maalum ya kubebea taka taka za hospitali na kupelekea mrundikano wa taka hasa mazalia na uwepo wa harufu mbaya katika eneo la Hospitali.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati imebaini kuwa hospitali ya wagonjwa wa akili inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa ufumbuzi wa haraka. Hivyo Kamati inaitaka Wizara kuunda idara maalum itakayoshughulikia afya ya akili na tiba ya madawa ya kulevya. Kufanya hivyo kutapelekea kuimarika kwa tiba ya akili na tiba ya madawa ya kulevya na kuondoa usumbufu uliopo sasa.

2. Kamati inaitaka Wizara kufanya ununuzi wa tanuri la kuchomea taka taka za hospitali (incinerator), ununuzi wa sehemu iliyobakia ya DNA mashine, ununuzi wa kifaa cha kupima damu za watoto ambao wamezaliwa na mama walioambukizwa VVU na kufanya tathmini ya vifaa vilivyokosekana katika hospitali ya Mnazi mmoja ili hatimae Wizara iweze kuweka vipaumbele vya kununua vifaa vilivyokosekana na kuondosha kasoro zinazojitokeza.

3. Kamati inaitaka Wizara kukiboresha Kitengo cha Takwimu cha Hospitali ya Mnazi mmoja pamoja na kuwafanyia utaratibu wa kupata eneo jengine ambalo watalitumia

katika kutunza kumbukumbu za wagonjwa vizuri kwani eneo lilipo sasa limekuwa finyu na mafaili ya wagonjwa yanashindwa kupangwa katika utaratibu mzuri.

4. Kamati inaitaka Wizara kuifanyia matengenezo Hospitali ya Mwembeladu katika sehemu ya huduma kwa walioambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU) kwani Kamati ilibaini kuwa walioambukizwa Virusi vya Ukimwi hupata huduma katika eneo la wazi hali inayoleta usumbufu.

5. Kamati inaitaka Wizara kuipatia Hospitali ya Mwembeladu madaktari ili waweze kusaidia katika huduma zinazotolewa na pia kuvifanyia matengenezo vifaa vya Hospitali ili viweze kutumika kwa ufanisi.

6. Kamati inaitaka Wizara kuipatia walinzi Hospitali ya Mwembeladu kutokana na kuwa wafanyakazi wengi waliopo ni wanawake na wamekuwa hawana usalama wa kutosha.

7. Kamati inaitaka Wizara kuiwekea Hospitali ya Mwembeladu Gari maalum la kubebea taka taka za Hospitali ili kuondokana na tatizo la kurudikana kwa mataka na harufu mbaya katika eneo la hilo.

TAASISI MAALUM ZA WIZARA YA AFYA.

1. CHUO CHA TAALUMA ZA SAYANSI ZA AFYA.
2. BODI YA USHAURI WA HOSPITALI BINAFSI.
3. BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI.
4. BARAZA LA TIBA ASILIA NA TIBA MBADALA.
5. BARAZA LA WAUGUZI.

CHUO CHA TAALUMA ZA SAYANSI YA AFYA.

Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya ni chuo pekee cha Serikali ambacho kinachotambulika kisheria Zanzibar kwa ajili ya kutoa mafunzo ya taaluma za Sayansi za Afya kwa kiwango cha stashahada katika kada ya uuguzi(general nursing), wasaidizi madaktari (clinical Officer), maafisa afya ya jamii na mazingira (environmental health sciences), ufundi sanifu wa maabara (medical laboratory sciences), wasaidizi madaktari wa afya ya kinywa na meno (dental therapy),ufundi sanifu wa madawa (pharmaceutical Technicians) na ufundi sanifu wa vifaa vya tiba (biomedical engineering).

Kamati ilipotembelea chuo ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya chuo pamoja na kugundua changamoto mbali mbali.

CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI CHUO CHA TAALUMA ZA SAYANSI YA AFYA.

1. Kuwepo kwa Mgogoro wa ardhi na uvamizi wa maeneo ya chuo kunakopelekea maeneo ya chuo kuzungukwa na makaazi ya watu na pia kuyafanya maeneo ya asili kupungua kila leo.

2. Upungufu wa walimu katika kada ya wasaidizi madaktari, kada ya madaktari wa meno na kada ya wafamasia. Kutokana na upungufu uliopo walimu huchukua jitihada ya kufundisha wanafunzi wengi tofauti na kiwango cha kawaida.

3. Darasa la ufundi Sanifu wa Vifaa vya Tiba (biomedical engineering) linakabiliwa na tatizo la kukosa huduma ya mtandao hali inayowakosesha wanafunzi fursa ya kujitafutia taaluma zaidi katika masomo yao.

4. Pia darasa linakosa usafiri wa uhakika pindi wanafunzi wanapohitaji kutoka nje kwa ajili ya masomo ya vitendo (field studies).

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuwaendeleza walimu waliopo chuo cha taaluma za sayansi kielimu na kuongeza walimu wengine wenye sifa ili kuondoa kasoro zilizopo na hatimae kutoa wahitimu watakaokuwa na sifa katika kada mbali mbali zinazotolewa chuoni hapo.

2. Kamati imesikitishwa sana na hali ya uvamizi wa maeneo na mgogoro wa ardhi uliopo katika eneo la chuo hivyo Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo kuhakikisha kuwa maeneo yote ya asili ya chuo yanapatikana.

3. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha darasa la ufundi sanifu wa vifaa vya Tiba(biomedical engineering)na kuitaka Wizara kuweka fungu maalum la fedha kwa ajili ya kuvifanyia matengenezo vifaa vya Hospitali (maintainance), kwani Kamati imebaini kuwa Serikali hutumia fedha nyingi kwa kununua vifaa vya hospitali lakini baada ya vifaa hivyo kununuliwa kunakuwa hakuna matengenezo ya mara kwa mara yanayofanyika kwa vifaa hivyo hali inayopelekea mpaka vifaa kufikia kuharibika ama kufa kabisa.

BODI YA USHAURI WA HOSPITALI BINAFSI.

CHANGAMOTO INAYOZIKABILI BODI YA USHAURI WA HOSPITALI BINAFSI.

Bodi inakabiliwa na changamoto ya fedha, usafiri na kushindwa kujitegemea na kujipangia kazi zake kwa mujibu wa mahitaji. Bodi hushindwa kufanya ukaguzi wa hospitali mbali mbali ambapo kwa kawaida hospitali zingelihitaji kufanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuona mazingira ya hospitali hizo pamoja na mapungufu yaliyopo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Afya kuisaidia Bodi kifedha ili iweze kujitegemea na hatimae kufanya kazi zake mbali mbali kwa ufanisi. Aidha Wizara iipatie Bodi usafiri wake binafsi ili iweze kujipangia kazi za ukaguzi katika hospitali na vituo vya afya.

BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI.

CHANGAMOTO INAYOZIKABILI BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI.

1. Kukosa ruzuku kutoka Serikalini.
2. Kuwepo kwa bandari zisizorasmi na kupelekea kuzagaa kwa bidhaa zisizo na viwango.
3. Kughushiwa kwa bidhaa na nyaraka kunakofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu.
4. Upungufu wa wafanyakazi wataalamu.
5. Uwepo wa ghala zisizosajiliwa.
6. Uelewa mdogo wa jamii juu ya kazi zinazodhibitiwa na bodi.
7. Bodi kupata mashirikiano madogo kutoka vyombo vya usimamizi wa sheria na wafanyabiashara.
8. Kuingizwa kwa bidhaa zisizofaa kwa matumizi.
9. Jengo la Ofisi halipo katika hali ya kuridhisha.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Bodi ruzuku ili iweze kutekeleza shughuli zake mbali mbali kwa ufanisi zaidi na kuweza kuilinda jamii ya kizanzibari.

2. Kamati inaitaka Wizara kuipatia Bodi fedha za kumaliza ujenzi wa Afisi ya Bodi mpya iliyopo Mombasa.

3. Kamati inaitaka Wizara kuifanyia marekebisho Sheria ya chakula, dawa na vipodozi ya mwaka 2006 ili iwe mamlaka ya chakula, dawa na vipodozi.

BARAZA LA TIBA ASILIA NA TIBA MBADALA.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI BARAZA LA TIBA ASILIA NA TIBA MBADALA.

1. Tatizo la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Baraza.

2. Kukosekana kwa akaunti ya Baraza kwa ajili ya kuwekea fedha zitakapopatikana kutoka kwa waganga wanapokwenda kusajili au fedha zinazotoka Wizarani.

3. Kutokuwepo kwa posho la mazingira hatarishi (risk allowance) kwa wakaguzi ambao hufanya ukaguzi katika mazingira tofauti yakiwemo mazingira ya hatari.

4. Baraza kukosa msaada au kutosikilizwa matatizo yao na Wizara kwasababu hakuna muamko kuhusu tiba asili katika kurugenzi zilizopo Wizarani.

5. Baraza kuingizwa katika MTEF lakini kutonufaika na chochote.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuwa karibu na Baraza pamoja na kuwasikiliza matatizo yao mbali mbali ili uwepo wa Baraza uwe ni kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya tiba asilia nchini na kuwafanya wafanyakazi wa Baraza hilo kujisikia kuwa ni sehemu ya wafanyakazi wa Wizara na pia kupatiwa miongozo mbali mbali pindi wanapohitaji.

2. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa Baraza linafunguliwa akaunti yake maalum kwa ajili ya urahisi wa kuhifadhi fedha zake.

BARAZA LA WAUGUZI.

CHANGAMOTO INAYOZIKABILI BARAZA LA WAUGUZI.

1. Kukosekana kwa bajeti ya kuendesha shughuli za Baraza kumepelekea kutokukamilika kwa kazi za Baraza kama vile kutokufanyika kwa vikao vya kawaida vya Baraza kwa zaidi ya miaka kumi na wajumbe wa Baraza kushindwa kufanya maamuzi ya pamoja. Pia Baraza linashindwa kutoa miongozo ya maadili kwa wauguzi.

2. Kukosa kushiriki mikutano ya kitaifa na kimataifa kama vile international council of nurses kutokana na kuwa Tanzania Bara wanawakilisha Baraza la Wauguzi kwa Tanzania nzima licha ya kuwa afya si miongoni mwa mambo ya muungano.

3. Ushirikishwaji mdogo wa watendaji wa Baraza la Wauguzi katika mambo muhimu yanayowahusu wauguzi kama vile ajira zinazohusiana na kada za uuguzi.

4. Sheria ya Baraza la Wauguzi na Wakunga kupitwa na wakati.

5. Ukosefu mkubwa wa vitendea kazi muhimu kwa wauguzi kunakopelekea kushuka hadhi ya uuguzi.

6. Ucheleweshaji wa ajira za wauguzi na wakunga kunapelekea wahitimu hao waliosomeshwa na Serikali kwenda kujitafutia ajira sehemu nyengine na huku hospitali zetu kukosa wataalamu hao.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kufuatilia upatikanaji wa bajeti ya Baraza kama ilivyopangwa ili Baraza liweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuendesha vikao, ufuatiliaji na tathmini kuhusiana na Baraza.

2. Kamati inaishauri Wizara kutafuta mbinu za kushiriki mikutano ya kitaifa na kimataifa Baraza la Wauguzi Zanzibar ili liweze kuenda sambamba na mabadiliko ya ukuaji wa taaluma za uuguzi duniani kwa kubadilishana uzoefu.

3. Kamati inaitaka Wizara kuharakisha kukamilika kwa Sheria mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga ili Baraza liwe na mamlaka kamili ya kufanya kazi zake na pia kuweza kutatua changamoto zilizopo katika Baraza.

OFISI ZA TIMU ZA AFYA ZA WILAYA.

Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilipata nafasi ya kukutana na Ofisi za Timu za Afya za Wilaya zilizopo Unguja ambazo ndio kiungo muhimu baina ya Wizara ya Afya na Wilaya. Kiujumla Ofisi hizo zipo Wilaya ya Kaskazini "A", Wilaya ya Kaskazini "B", Wilaya ya Kati, Wilaya ya Kusini, Wilaya ya Mjini na wilaya ya Magharibi.

Miongoni mwa majukumu ya Ofisi hizo ni kusimamia kazi zote za huduma za afya katika Wilaya, kufanya ukaguzi wa huduma mbali mbali za afya zinazotolewa ndani ya Wilaya, uchukuaji wa dawa na vifaa kutoka Bohari Kuu ya Madawa na kuvisambaza vituoni na kuandaa, kupanga mpango kazi wa mwaka wa Wilaya na utekelezaji wake.

CHANGAMOTO WANAZOZIKABILI OFISI ZA TIMU ZA AFYA ZA WILAYA.

1. Uchakavu wa magari ya Ofisi za Timu za Afya za Wilaya na kupelekea kukosa usafiri wa uhakika katika kufuatilia shughuli zao mbali mbali jambo ambalo limepelekea Ofisi kutumia bajeti kubwa katika kutengeneza magari mara kwa mara.

2. Upungufu wa Dawa katika Vituo vya Afya na zinapopatikana zinakuwa hazitoshi na pia zinakuwa zinakaribia kuisha muda wa matumizi.

3. Kukosekana kwa posho la dhamana kwa Watendaji wa Timu za Afya za Wilaya na katika marekebisho ya mishahara yaliyofanywa Serikalini "risk allowance" haikutolewa kwa watendaji wa Timu za afya za Wilaya .

4. Ukosefu wa maji katika vituo vya afya. Miongoni mwa vituo vinavyokosa huduma ya maji ni kituo cha Afya cha Bwefum, Shakani, Gamba, Mkokotoni, Matemwe, Misufini, Donge, Miwani, Machuwi, Unguja Ukuu, Uzi, Cheju, Pwani Mchangani, Tazari na Ndijani Mseweni.

5. Uchakavu wa nyumba za madaktari ambapo miongoni mwa vituo vyenye tatizo hilo ni kituo cha Chaani Masingini na Gamba; uchakavu wa vituo vya Afya kama kituo cha Kiboje, Tunguu, Umbuji, Ndijani Mseweni,Chaani Masingini, Chaani Kubwa na upungufu wa nyumba za wafanyakazi katika maeneo ya Kijini, Chaani Kubwa, Masingini, Matemwe, Pwani Mchangani na Nungwi.

6. Deni kubwa la umeme kwa wakaazi wa nyumba za afya vituoni ambapo wakaazi hao hushindwa kulipa na kukaa giza. Pia kutokana na mabadiliko yanayofanywa na Shirika la Umeme la kubadilisha mita, na limbikizo la deni lilokuwepo kubakia vile vile hata kama mkaazi atakuwa mwengine ambapo wakaazi wa nyumba hizo wamejikuta wakilazimishwa kuzilipia mita ambazo madeni yake yametokana na kurithi.

7. Upungufu wa vifaa katika vituo. Miongoni mwa vifaa vilivyokosekana katika vituo vingi ni vifaa vya meno na vifaa vya maabara.

8. Fedha kutoingia kwa wakati na kukwamisha shuguli zilizopangwa.

9. Upungufu wa wafanyakazi katika vituo vya afya kwa kada mbali mbali kama vile madaktariwasaidizi, wauguzi wakunga, mabwana/mabibiafya, wafamasia wasaidizi, maodali n.k.

10. Kutokupata ajira kwa wahudumu wanaojitolea wanaokuwepo katika maeneo ya karibu.

11. Usalama mdogo wa vituo pamoja na Ofisi za Afya za Wilaya kutokana na kukosekana kwa uzio na ulinzi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kulitafutia ufumbuzi tatizo la usafiri kwa timu za Afya za Wilaya ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na kuepuka kutumia bajeti yao katika kufanya matengenezo ya mara kwa mara.

2. Katika kupunguza tatizo la upungufu wa dawa na vifaa Kamati inaishauri Wizara kuanzisha kisheria utaratibu wa kuchangia huduma za afya hasa tukizingatia kwasasa mara nyingi watu hulazimika kununua madawa na vifaa wanavyoandikiwa ambapo ingekuwa ni wepesi kama utaratibu wa kuchangia huduma ungekuwepo.

3. Kamati inaitaka Serikali kubeba gharama za malipo ya mita za umeme pamoja na malimbikizo ya madeni yake ili wafanyakazi wanaoendelea kukaa katika nyumba za vituo vya afya waondokane na kulipa madeni ya kurithi na pia Serikali iandae utaratibu mzuri wa kulipa umeme katika nyumba na vituo vya afya.

4. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara bajeti ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa ili hatimae Wizara iweze kuvipatia vituo vya afya dawa na vifaa kwa wakati ambazo zitaweza kutumika kwa muda mrefu kabla ya kumaliza muda wake na pia Kamati inaiomba Wizara kuwapatia posho la dhamana watendaji wa Timu za Afya za Wilaya.

5. Kamati inaishauri Wizara kuandaa utaratibu wa kuweka ulinzi katika vituo vya afya kwa kuwatumia wanajamii wenyewe waliopo katika maeneo ya vituo ili kupunguza wizi na uharibifu wa vifaa.

6. Kamati inaishauri Wizara kuzihushisha Timu za Afya za Wilaya katika kufanya uteuzi wa wafanyakazi wasio wataalamu wa afya (supporting staffs) katika sehemu husika hasa

hasa kwa sehemu za mashamba ili kupunguza matatizo yanayojitokeza ikiwemo kukosa nafasi za ajira kwa wahudumu wanaojitolea.

WIZARA YA UWEZESHAJI, USTAWI WA JAMII, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO.

Wizara imeundwa katika Idara zifuatazo:-

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
3. Idara ya Ustawi wa Jamii.
4. Idara ya Maendeleo ya Vijana.
5. Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto.
6. Idara ya Mikopo.
7. Idara ya Ushirika.
8. Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji kiuchumi.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Idara ya Mipango Sera na Utafiti ni kiungo kikubwa katika Wizara na miongoni mwa majukumu ya Idara hii ni kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Mipango, Miradi na Programu za Maendeleo za Wizara. Kamati ilielezwa kuwa Idara imeendelea kutekeleza shughuli zake mbali mbali ikiwemo kuzisimamia Kamati za shehia zinazoshughulikia maswali ya kuzuia na kupinga vitendo dhidi ya udhalilishaji.

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI KAMATI ZA SHEHIA ZINAZOSHUGHULIKIA MASWALI YA KUZUIA NA KUPINGA VITENDO DHIDI YA UDHALILISHAJI.

1. Kukosekana kwa ushahidi wa kesi zinazoripotiwa polisi na Kamati za Shehia zinazoshughulikia maswali ya kuzuia na kupinga vitendo dhidi ya udhalilishaji. Kamati hizo zimekuwa na masikitiko makubwa juu ya kesi zinazokosa ushahidi kwani zinarudisha nyuma jitihada za Kamati pamoja na jamii kukosa suluhisho na sehemu ya kukimbilia dhidi ya kesi za udhalilishaji.

2. Kamati kukosa mchango wa fedha kutoka Wizarani kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao hali inayopelekea wajumbe kulazimika kuchangia fedha pindi

panapotokea matumizi yeyote. Kamati zimekuwa zikipatiwa mafunzo pekee na Wizara kwa lengo la kuziwezesha kutatua changamoto zinazojitokeza katika jamii zao ikiwemo udhalilishaji, ubakaji, mimba za utotoni nakadhalilka.

3. Kamati kukosa maeneo maalum katika kufanya shughuli zao.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuishajihisha jamii kushiriki kikamilifu katika kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili zipatiwe ufumbuzi.

2. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kuzisimamia Kamati za Shehia zinazoshughulikia maswali ya kuzuia na kupinga vitendo dhidi ya udhalilishaji, kuzishajihisha kupata maeneo yao rasmi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao na kuziwezesha kifedha pindi kunapotokea mahitaji ya msingi.

IDARA YA USTAWI WA JAMII.

Kamati ilielezwa kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii inaendelea kufanya kazi zake za kawaida za kuhakikisha kuwa huduma za kiustawi zinatolewa kwa watoto na wazee wanaoishi katika mazingira magumu.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA USTAWI WA JAMII.

1. Kuwepo kwa deni la fidia la wafanyakazi 71 walioumia kazini lenye thamani ya Tshs milioni 92,844,586/= (Unguja Shilingi 32,560,064/= na Pemba Shilingi 60,284,522/=) ambapo ni mzigo mkubwa kwa Idara.

2. Vituo vya Mkono kwa Mkono vinakabiliwa na ufinyu wa nafasi pamoja na usafiri kwa ajili ya kutembelea shehia mbali mbali.

3. Kamati za shehia za kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zinakabiliwa na changamoto ya mwamko mdogo kwa jamii katika kuchangia mfuko wa Kamati hali inayokwamisha maendeleo ya Kamati hizo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kuwapa ushirikiano wa karibu Wizara ya Fedha ambao waliahidi kulipa deni lote la fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini kabla ya kufika mwishoni mwa mwezi wa Machi 2014 baada ya kukamilisha baadhi ya taratibu ikiwemo uhakiki wa madeni ya wanaodai fidia.

2. Kamati inaitaka Wizara kuvipatia vituo vya mkono kwa mkono usafiri wa uhakika ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kutembelea shehia mbali kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii.

3. Kamati inaishauri Wizara kutoa Elimu kwa Jamii juu ya umuhimu wa Kamati za Shehia za Kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ili wanajamii waweze kushajihika katika kuzichangia kamati hizo.

CHANGAMOTO WANAZOZIKABILI NYUMBA YA KULELEA WATOTO MAZIZINI.

1. Kamati iliarifiwa kuwa kuna tatizo la usafiri na pia wafanyakazi wanalipwa malipo madogo na Serikali ambayo hayakidhi haja.

2. Wafanyakazi wanaowahudumia watoto hawana ujuzi wa kuwalea watoto ambao watakuwa na mahitaji maalum pindi watakapoletwa katika nyumba ya kulelea watoto.

3. Upungufu wa wafanyakazi hasa wa kada za chini kama vile wasafishaji na upungufu huo husababisha kazi kutokufanyika kwa ufanisi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuwapa mafunzo wafanyakazi wanaolea watoto wenye mahitaji maalum ili waweze kulea watoto wa aina tofauti.

2. Kamati inaitaka Wizara kuajiri wafanyakazi wa kada za chini kwa ajili ya nyumba ya kulelea watoto Mazizini kwani msafishaji aliepo hivi sasa ni mmoja tu.

CHANGAMOTO WANAZOZIKABILI NYUMBA YA WAZEE SEBLENI.

1. Ukosefu wa usafiri kwa ajili ya kufanikisha shughuli mbali mbali katika nyumba hiyo kama vile kuwapeleka wazee hospitali.

2. Upungufu wa wafanyakazi wa kada za chini kama vile wasafishaji na walinzi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kulitafutia ufumbuzi suala la usafiri kwa ajili ya nyumba ya wazee sebleni ili waweze kurahisisha mahitaji ya wazee waliopo nyumba hiyo.

2. Kamati imeridhishwa sana na juhudi za Wizara za kuyafanyia matengenezo nyumba za wazee Sebleni hivyo inaitaka Wizara kuzipatia nyumba hizo wahudumu wa kutosha ili nyumba hizo ziweze kutunzwa kama inavyohitajika.

IDARA YA URATIBU NA UENDELEZAJI WA PROGRAM ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.

Idara hii ina jukumu la kubuni na kuratibu programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuwawezesha kujiajiri na kuwa na kipato endelevu cha kuweza kumudu maisha yao kwa malengo ya kumiliki uchumi wao, kuchangia maendeleo ya nchi. Kamati ilitembelea Idara hii na kupokea taarifa juu ya utendaji wa shughuli zake.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA UWEZESHAJI.

1. Ufinyu na uhaba wa vitendea kazi kama vile computa.

2. Uelewa mdogo wa dhana ya uwezeshaji kwa jamii.

3. Mahitaji ya uwezeshaji kwa wananchi ni mengi ukilinganisha na uwezo wa Serikali katika kutoa huduma za uwezeshaji ambazo zitawapa uwezo wajasiriamali katika kujiendeleza.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya dhana ya uwezeshaji kupitia vyombo habari ili hatimae jamii ipate ufahamu na kuweza kujishughulisha katika kazi mbali zitakazowakwamua kiuchumi.

2. Kamati inaishauri Wizara kuandaa mikakati mbali ya kuwapatia mahitaji wajasiri amali na masoko ya uhakika ili fedha zinazotumiwa na Serikali katika kuwawezesha zitumike ipasavyo.

IDARA YA USHIRIKA

Idara ya Ushirika ina jukumu la kusajili na kuendeleza vyama vya ushirika Zanzibar kupitia mrajisi wa vyama vya ushirika, aidha kufanya ukaguzi wa hesabu wa vyama hivyo na kutoa ushauri pale inapohitajika.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA USHIRIKA.

1. Kamati iligundua kuwa Idara ya ushirika inakabiliwa na tatizo la uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma hasa kwenye fani za ukaguzi, masjala, ufuatiliaji na tathmini.

2. Kamati imesikitishwa na Ofisi ya Idara ya Ushirika kwani ni chakavu na haitoshelezi kwa mahitaji ya Idara husika, aidha Kamati iliarifiwa kuwa tayari wamepata jengo eneo

la Migombani kwa ajili ya Ofisi, jengo ambalo linahitaji matengenezo makubwa kabla ya kuhamiwa.

3. Ukosefu wa usafiri wa uhakika; Idara bado inakabiliwa na tatizo la usafiri jambo linalokwamisha ufanisi wa kazi zao za ufuatiliaji wa vyama vya ushirika.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuwapatia Idara fedha kwa ajili ya kulifanyia matengenezo jengo lao kongwe walilopatiwa ili waweze kuhamia na kufanya kazi zao kwa ufanisi.

2. Kamati inashauri kupatiwa kwa Idara hii usafiri wa uhakika ili waweze kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kufuatilia vyama vya ushirika.

3. Kamati inaitaka Wizara kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Idara hii ili wawe na taaluma juu ya masuala wanayoyafanyia kazi, Mafunzo hayo yajumuishe mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

IDARA YA MIKOPO

Idara ya Mikopo ina jukumu la kuendesha taasisi ya fedha ambayo itasaidia wananchi kwa kuwapatia mitaji kupitia mikopo nafuu na huduma za ushauri ili kuwawezesha kufanya shughuli za uzalishaji na kunyanyua hali zao za maisha na kiuchumi.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA MIKOPO.

1. Kamati ilielezwa kuwa kuna upungufu wa wafanyakazi.

2. Idara inakabiliwa na wafanyakazi wenye utaalamu mdogo katika masuala ya mikopo.

3. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika.

4. Ufinyu wa Ofisi ambazo hazitoshelezi kwa ufanisi wa kazi.

5. Jamii imekuwa na mtazamo hasi juu ya Mifuko inayosimamiwa na asasi za Serikali.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Wizara kuwapatia Idara ya Mikopo wafanyakazi wa kutosha na wenye sifa ili kufanikisha kazi zao kwa ufanisi.

2. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia Idara ya Mikopo Ofisi itakayokidhi mahitaji yao kwani Ofisi waliyopo hivi sasa hairidhishi.

3. Kamati inashauri kupatiwa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara ya Mikopo ili wafanye kazi zao kwa utaalamu zaidi.

4. Kamati inaitaka Idara kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa inatoa elimu kwa wananchi juu ya masuala ya mikopo.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni miongoni mwa Wizara ambazo kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inazisimamia kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Wizara hii imekusanya idara na Taasisi zifuatazo:-

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
3. Idara ya Elimu ya Maandlizi na Msingi.
4. Idara ya Elimu ya Sekondari.
5. Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu.
6. Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.
7. Idara ya Mafunzo ya Ualimu.
8. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu.
9. Taasisi ya Elimu Zanzibar.
10. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.
11. Taasisi ya Elimu ya Juu.
12. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
13. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.
14. Baraza la Mitihani la Zanzibar.
15. Bodi ya Huduma za Maktaba.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipata nafasi ya kuzikagua na kuzitembelea baadhi ya idara na taasisi zilizo chini ya Wizara ya elimu na Mafunzo ya Amali kwa lengo la kuangalia uendeshaji wake wa kazi, miongoni mwa idara hizo ni kama ifuatavyo:-

OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU

Hii ni miogoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambapo ni taasisi muhimu katika maendeleo ya elimu nchini, ukaguzi ni jambo linaloboresha elimu kwa kupitia wakaguzi ambao hufanya kazi katika mazingira magumu sana.
Malengo makuu ya ofisi hii ni kuhakikisha utowaji na upatikanaji wa elimu bora katika ngazi zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari. Baada ya ukaguzi walimu na walimu wakuu hushauriwa na kuelekezwa namna bora zaidi za kuzipatia skuli zao maendeleo endelevu.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU

1. Uchache wa fedha za bajeti: Kamati imebaini kuwa shughuli nyingi za Idara ya ukaguzi wa elimu hazina fedha za kutosha kwa ajili ya kufanikisha kazi za ukaguzi, katika mwaka huu wa fedha ofisi ina malengo ya kuzikagua skuli 342 zikiwemo skuli za serikali na za binafsi, lakini changamoto iliyopo ni bajeti finyu ambayo haikidhi mahitaji.
2. Kuongezwa kwa maposho ya wakaguzi: Kamati imejiridhisha kuwa wakaguzi wanakazi ngumu za kukagua skuli zetu na wanafanyakazi katika mazingira magumu sana bila ya kuangaliwa kwa maslahi yao hivyo Kamati inaitaka Wizara kuangalia upya maslahi ya Wakaguzi.
3. Utoro kwa wanafunzi: Kamati imebaini kuwa tatizo la utoro bado ni changamoto kubwa katika skuli zetu za Unguja na Pemba hali inayopelelekea ufaulu mdogo kwa wanafunzi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri kulipa kipaumbele suala la ukaguzi wa elimu kwa kuwatengea bajeti ambayo itakidhi mahitaji ya ukaguzi kwani sekta ya elimu inategemea sana wakaguzi ili iweze kupata mafanikio.

2. Kamati inashauri Wizara katika kukabiliana na tatizo la utoro katika skuli zetu kuwashajihisha walimu ikiwa ni pamoja na walimu wakuu kudhibiti suala la utoro kwa kushirikiana na wazee pamoja na kamati za Skuli.

3. Kamati inaagiza kuongezewa maposho wakaguzi kwani wanafanyakazi katika mazingira magumu katika kutekeleza majukumu yao ya ukaguzi.

4. Kamati inaitaka Wizara kuwapatia jengo la ofisi wakaguzi wa Pemba kwani ofisi wanayotumia hivi sasa hairidhishi hata kidogo ukilinganisha na umuhimu wa ofisi yenyewe katika maendeleo ya elimu.

5. Kamati inaagiza kuwapatia usafiri Ofisi ya mkaguzi Mkuu wa elimu kwa ofisi ya Pemba kwani usafiri bado ni changamoto kubwa katika kufanikisha kazi zao za kila siku.

IDARA YA ELIMU YA MAANDLIZI NA MSINGI

Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi ina jukumu ya kusimamia utoaji wa elimu bora kwa ngazi ya maandalizi na msingi pamoja na uratibu wa elimu katika vyuo vya kur-ani na madrasa hapa nchini, Aidha husimamia skuli binafsi za maandalizi na msingi, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati ilibahatika kutembelea baadhi ya vitengo ambavyo vimo katika Idara hii kama ifuatavyo.

SKULI ZA MAANDALIZI.

Kamati katika kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Baraza la wawakilishi na katika kutaka kujiridhisha ilitembelea baadhi ya Skuli za maandalizi, Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali katika kujenga na kuziimarisha Skuli za maandalizi hii inadhihirisha ni jinsi gani elimu ya maandalizi inavyopewa kipaumbele kwa kuifanya kuwa ni elimu ya lazima, mfano wa Skuli hizo ni Skuli ya maandalizi Msuka (Ungi).

ZANZIBAR MADRAS RESOURCE CENTRE.

Ni programu inayosaidiwa na Aga Khan Foundation ambayo ilianzishwa mwishoni mwa mwaka 1980 ambayo kazi yake kubwa ni kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa maendeleo na makuzi ya watoto, kuandaa walimu wa maandalizi, kuandaa mtaala wa Skuli za maandalizi pamoja na kutoa mafunzo na kuandaa vifaa vya kufundishia.
Kituo hiki kinashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuimarisha na kuendeleza elimu ya maandalizi nchini.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI.

1. Kukosekana kwa sera ya pamoja juu ya maendeleo na makuzi ya mtoto (early Childhood Development):Kamati imebaini kuwa sera yetu ya elimu bado haijatambua rasmi mpango wa maendeleo na makuzi ya mtoto na bado haijapewa kipaumbele kwa lengo la kuimarisha mitaala katika skuli za maandalizi.

2. Kukosekana kwa posho kwa walimu wa skuli za maandalizi za jamii: ni dhahiri kuwa skuli za maandalizi za jamii bado ni changa hivyo walimu wanaofundisha katika skuli hizo hufanya kazi zaidi kwa kujitolea bila ya kupata angalau pesa ya usafiri kwa ajili ya kazi hiyo ya kutumikia jamii.

3. Bajeti finyu: Kamati imejiridhisha kuwa fedha za bajeti zinazotengwa kwa ajili ya Idara hii ni chache ukilinganisha na majukumu mazito inayopangiwa ikiwa ni pamoja na kusimamia elimu ya msingi na maandalizi.

4. Uhaba wa walimu katika Skuli za Msingi: tatizo la upungufu wa walimu bado ni changamoto katika skuli za msingi hasa ukilinganisha na idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kila mwaka jambo ambalo hupelekea walimu kuwa na wakati mgumu kufundisha idadi kubwa ya wanafunzi katika madarasa.

5. Uhaba wa vikalio (madawati): Kamati imejiridhisha kuwa bado baadhi ya skuli za Unguja na Pemba za Msingi zina ukosefu wa madawati hali inayopelekea wanafunzi kuendelea kukaa chini wakati wa masomo yao.

6. Ukosefu wa hatimiliki za maeneo yaliyojengwa Skuli: Kamati imebaini kuwa Skuli nyingi hazina hatimiliki ya eneo ambalo skuli hiyo imejengwa na kupelekea uvamizi wa maeneo hayo pamoja na migogoro baina ya wananchi. Miongoni mwa Skuli hizo ni skuli ya Fuoni Kitongani.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaagiza Wizara kuwa elimu ya maendeleo na makuzi ya mtoto ipewe kipaumbele Serikalini ili wanafunzi wasomeshwe masomo hayo yatakayojumuisha Afya,elimu, ustawi, kinga, lishe n.k).
2. Kamati inaagiza Serikali iandae mkakati maalum wa maendeleo na makuzi ya Mtoto, yaani early Childhood Development (ECD) framework na iwashirikishe wadau wote ikiwa ni pamoja a Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara inayoshughulikia ustawi wa Jamii na watoto, Wizara ya kilimo pamoja na Wizara ya Fedha.
3. Kamati inaishauri Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi itengewe fedha za kutosha kwa ajili ya kufanikisha kazi zake.
4. Kamati inashauri kuwa dhana ya Ushirikiano baina ya Serikali na Sekta binafsi iimarishwe.
5. Kamati inashauri Wizara kuwapatia walimu wanaofundisha skuli za maandalizi za jamii posho la angalau 20,000 kwa mwezi ili kuwapa motisha katika kazi zao.
6. Kamati inaitaka Wizara kujipanga vizuri zaidi katka kuhakikisha kuwa wanazipatia Skuli zote za Unguja na Pemba madawati kwa ajili ya wanafunzi kwani utaratibu wa kukaa chini umeshapitwa na wakati na unarudisha nyuma maendeleo ya elimu.
7. Kamati imesikitishwa sana na tatizo la upungufu wa walimu katika Skuli za Msingi hivyo Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kulipatia ufumbuzi tatizo hili kwani kuna idadi kubwa ya wahitimu walimu wa elimu ya msingi ambao wamekosa ajira kwa kipindi kirefu.
8. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa na hatimiliki za maeneo ya skuli ili kudhibiti suala la uvamizi wa maeneo ambalo limekithiri katika maeneo mengi ya skuli za Unguja na Pemba.

IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI

Idara ya elimu ya Sekondari inajukumu la kusimamia utekelezaji kazi za ufundishaji kwa ujumla na ufuatiliaji wa utendaji kazi maskulini, kupanga walimu katika skuli zote za

Serikali za sekondari na kuwapangia skuli wanafunzi waliofaulu katika ngazi mbali mbali za elimu.

Elimu ya Sekondari kwa mwaka 2012/2013 imetolewa kwa Skuli zipatazo 252 kati ya hizo skuli 205 ni za Serikali na 47 ni za Binafsi.

SKULI YA UFUNDI KENGEJA.

Skuli ya ufundi Kengeja ni miongoni mwa skuli zinazotoa elimu ya ufundi Zanzibar, Skuli hii imeanzishwa mwaka 1994 ambapo ufundi unaotolewa skulini hapo ni pamoja na civil engineering(ufundi uwashi) na electrical engineering(ufundi wa umeme).Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaipongeza Wizara kwa kuanzisha Skuli hii kwani inatoa wahitimu walio bora ambao huwa ni vijana wanaoweza kujiajiri wenyewe baada ya kumaliza masomo yao,aidha Skuli inafanya vizuri katika masomo ya ufundi.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA UFUNDI KENGEJA

1. Ukosefu wa dakhalia: Kamati imejiridhisha kuwa katika Skuli ya Kengeja kuwa kuna upungufu wa nyumba ya wanafunzi hususan wanafunzi wa kike, Kamati iliarifiwa kwamba kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Dakhalia hiyo tayari kipo lakini bado Wizara haijatenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo jambo ambalo linasababisha usumbufu mkubwa kwa wanafunzi.
2. Ukosefu wa baadhi ya vifaa katika workshop ya umeme: hii ni miongoni mwa changamoto iliyopo katiika Skuli ya ufundi Kengeja ambapo baadhi ya vifaa vya kufundishia masomo ya umeme vinakosekana.
3. Ukosefu wa Dereva: Kamati imesikitishwa sana na tatizo la kukosekana kwa dereva kwa ajili ya mahitaji ya skulini hapo jambo hili hupelekea kuzorotesha shughuli mbali mbali za skuli hiyo.
4. Ukosefu wa hatimiliki ya eneo la Skuli: Kamati imebaini kwamba Wizara kupitia Skuli ya kengeja bado hawajakabidhiwa hatimiliki ya eneo hilo, hali ambayo inapelekea wasi wasi wa kutokea uvamizi katika maeneo ya skuli.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaishauri Wizara kuitengea fedha katika bajeti ya 2014/2015 Skuli ya Ufundi kengeja kwa ajili ya kufanikisha Ujenzi wa Dakhalia ya Wanawake.
2. Kamati inaiagiza Wizara kuipatia Skuli ya Ufundi Kengeja vifaa vya kutosha kwa ajili ya workshop ya umeme ili wanafunzi wapate fursa ya kufanya mazoezi ya vitendo katika somo la umeme.

3. Kamati inaitaka Wizara kutoa ajira ya Dereva kwa ajili kurahisisha shughuli mbali mbali za Skuli hiyo.

TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

Taasisi hii ilianzishwa mnamo mwaka 2011 amapo miongoni mwa malengo makuu ya kuanzishwa kwake ni kutayarisha mitaala na vielelezo vya kufundishia kwa ajili ya kuongeza ubora wa elimu katika ngazi za maandalizi, msingi, Sekondari na vyuo vya ualimu. Pamoja na mambo mengine Taasisi ya Elimu hujikita katika kufanya utafiti wa kielimu kwa lengo la kuboresha mitaala katika elimu.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR.

1. Ukosefu wa fedha za kutosha: uingizwaji mdogo wa fedha za ruzuku zilizotengwa kwa ajili ya taasisi ya elimu unazorotesha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi.
2. Ukosefu wa vitendea kazi: Taasisi inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vitendea kazi kama vile Computa, viti nk kwani hivyo wanavyotumia kwa sasa vimeshachakaa kiasi cha kutokutumika tena katika kufanyia kazi zao za kila siku.
3. Ukosefu wa wafanyakazi wenye utaalamu unaohitajika katika Taasisi: Katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku Taasisi ya Elimu inakabiliwa na changamoto ya uchache wa wafanyakazi wenye taaluma inayohitajika kwa mujibu wa kazi za taasisi hii.
4. Ukosefu wa Ofisi za kutosha: Kamati imesikitishwa na ufinyu wa Ofisi ambazo Taasisi ya Elimu inafanyia kazi. Taasisi hiyo ingehitaji kupatiwa sehemu yenye nafasi ya kutosha ili iweze kufuatilia maendeleo ya elimu nchini kwa ufanisi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuingiza kwa wakati fedha za bajeti zilizoidhinishwa kwa matumizi ya Taasisi ya Elimu ili waweze kufanikisha majukumu na malengo yao waliyojipangia.
2. Kamati inaishauri Serikali katika mipango yao waliyojipangia ya ujengaji wa ofisi mbali mbali za Serikali kuwaangalia na kuwapa kipaumbele Taasisi ya Elimu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ujumla kwani ufinyu wa nafasi ni changamoto kwa Wizara nzima.
3. Kamati inashauri Wizara kuipatia Taasisi ya Elimu vitendea kazi ambavyo vitaendana na mahitaji halisi waliyonayo.

BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA

Bodi ya huduma za Maktaba ni Bodi inayoshughulikia na kusimamia uratibu wa usomaji wa vitabu katika maskuli na katika jamii kwa ujumla, miongoni mwa majukumu ya msingi ya Bodi za huduma za maktaba ni kuanzisha, kukuza na kuendesha maktaba

katika visiwa vya Zanzibar pamoja na kuanzisha na kuandaa vituo vya nyaraka na kutoa huduma za upatikanaji wa taarifa mbali mbali.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA.

1. Ufinyu wa bajeti: Bodi inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununulia vitabu sahihi na vinavyofaa kwa watumiaji wa maktaba na kufanikisha shughuli mbali mbali za bodi hiyo kama vile kufanya shughuli za kuhamasisha jamii kupenda kujisomea (book fairs, reading tents) uandaji wa sera na kujenga mitandao na maktaba nyengine.
2. Upungufu wa watendaji wenye taaluma: Kamati imebaini kuwa maktaba zetu hazina watendaji wenye taaluma hasa wakutubi, na hao watendaji waliopo katika maktaba zilizo katika maskuli hutoa huduma za maktaba bila ya kuwa na utaalamu wowote juu ya kazi hiyo kwani wengi wao ni walimu wa kawaida.
3. Upungufu wa vifaa vya maktaba na vitabu: maktaba nyingi zinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vitendea kazi ikiwemo samani mbali mbali na vitabu vya kusomea.
4. Muamko mdogo katika jamii:Kamati imebaini kuwa jamii bado haijawa na muamko wa kupenda kusoma vitabu na kuona umuhimu wa maktaba katika jamii zetu licha ya kuwa na maktaba za jamii katika baadhi ya maeneo.
5. Ukosefu wa usafiri: maktaba kuu inakabiliwa na tatizo la usafiri kwa ajili ya kuendesha shughuli mbali mbali za maktaba.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inaipatia Bodi ya huduma za maktaba usafiri wa uhakika ili waweze kufanikisha shughuli zao.
2. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuipatia Wizara ya Elimu na Taasisi zake kwa ujumla fedha za kutosha na kwa wakati kwani kucheleweshaji fedha hizo hupelekea kukwama kwa malego waliyojipangia.
3. Kamati inaishauri bodi ya huduma za maktaba kuchukua jitihada za makusudi katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kusoma vitabu kwani uelewa bado ni mdogo kwa wananchi walio wengi.
4. kamati inashauri kuanzishwa kwa wingi Maktaba za jamii ili huduma hizo ziwafikie wananchi kwa urahisi.
5. Kamati inashauri kuendelea na mpango wa maktaba za visanduku katika skuli mbali mbali ili huduma ya kujisomea vitabu ipatikane kwa wanafunzi mbali mbali nchini.
6. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Maktaba kuu Pemba kwani ni dhahiri kuwa huduma za maktaba kwa upande wa pemba zitakuwa bora na za uhakika tofauti na ilivyo sasa.
7. Kamati inashauri kutolewa mafunzo kwa wakutubi wa maskulini ili waweze kutoa huduma zao kwa utaalamu unaotakiwa.

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar ni miongoni mwa vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya juu nchini ambacho kinamilikiwa na Serikali, katika mwaka wa fedha 2012/2013.Chuo kimefanya mabadiliko ya mfumo wake na kuweka skuli nne badala ya kuwa na skuli moja hapo kabla, aidha idara na vitengo mbali mbali vimeanzishwa, skuli zenyewe ni pamoja na Skuli ya Elimu Endelezi na Utaalamu, Skuli ya Elimu, Skuli ya Kiswahili na Lugha za kigeni na Skuli ya Sayansi Asili na Jamii.

Kamati inakipongeza Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa kuhamia katika kampasi yake ya Tunguu aidha Kamati imejiridhisha juu ya Elimu inayotolewa chuoni hapo kwani Chuo kinatoa wahitimu hadi wa Sayansi ya Udaktari kwa sasa.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR.

Miongoni mwa changamoto ambazo chuo zinakabiliana nazo ni:-

1. Kutokukamilika kwa baadhi ya majengo: Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya majengo katika kampasi ya tunguu hayajakamilika kutokana na ukosefu wa fedha, majengo hayo ni ujenzi maabara, utiaji wa umeme katika baadhi ya maeneo na kuweka tiles.
2. Upungufu wa wahadhiri kwa baadhi ya program: Chuo Kikuu cha Taifa kinakabiliwa na upungufu wa wahadhiri na kutegemea zaidi walimu wa muda (Part time) ambapo chuo kinagharamika zaidi katika kuwapata.
3. Uhaba wa vitabu vinavyolingana na program zinazotolewa na chuo.
4. Uhaba wa ruzuku kutoka Serikalini: Chuo kikuu cha Taifa hupata ruzuku kutoka Serikalini ambapo ruzuku hiyo ni finyu na haitoshelezi katika kutekeleza majukumu mbali mbali ya Chuo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inashauri kukamilishwa kwa baadhi ya majengo katika chuo kikuu cha Taifa ili majengo hayo yaweze kutumika kama ilivyokusudiwa.
2. Kamati inashauri kuajiriwa kwa wahadhiri wa kufundisha kozi zote zinazotolewa chuoni hapo ili kuondokana na tatizo la kuwa na walimu wa muda.
3. Kamati inakitaka Chuo kikuu cha Taifa kutenga fedha maalum kwa ajili ya ununuzi wa vitabu hasa vile vitabu ambavyo vinatumika kwa kozi na masomo yanayotolewa chuoni hapo.
4. Kamati inaishauri Chuo Kikuu cha Taifa kubuni njia nyengine za kujiongezea mapato kwa lengo la kuendesha shughuli za chuo kwa ufanisi.

SEHEMU YA TATU

HITIMISHO

Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi - Zanzibar, Toleo la mwaka 2012. Kamati imetoa maelekezo na ushauri mbali mbali ambao utasaidia katika kutatua changamoto na kasoro tulizoziainisha na hatimae kuleta ufanisi zaidi katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na Wizara ya Uwezeshaji,Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Kiujumla Wizara zote ambazo Kamati inazisimamia zinakabiliwa na changamoto ya Uhaba wa Fedha hali inayochangia kukwamisha utekelezaji wa malengo ya Wizara husika, Hivyo Kamati inaisisitiza Serikali kuzipatia Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii fedha kwa mujibu wa Bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwani Kamati imegundua kuwa hata fedha chache ambazo Wizara hizi zinaidhinishiwa katika Bajeti yake ya mwaka huwa haziingizwi ipasavyo.

Kamati inatoa shukrani kwa watendaji wote wa Idara na Taasisi mbali mbali kwa mashirikiano yao waliyotupatia wakati wa kazi za Kamati na hatimae kufanikisha uandishi wa ripoti hii. Aidha, Kamati inatoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.